# TARGETER WINGS
# KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
# GREDI YA 6 - MWAKA WA 2026
# SEHEMU A:
# KISWAHILI LUGHA

Wings 001

**Muda: Saa 1**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha Kiswahili na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30.
2. Ukisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

**NAMBA YAKO YA TATHMINI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**
**JINA LA SOMO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali **1 - 30** umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu sahihi.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**
**Katika kijitabu cha maswali chagua jibu sahihi:**

29. Kamilisha methali:-
Mtoto umleavyo________________

A. hutazama kisogo cha nina  B. hulia kivulini
C. ndiyo akuavyo  D. hafi njaa

Jibu sahihi ni C.
**Katika karatasi ya majibu:**

**29.** [A] [B] [~~C~~] [D]  **30.** [A] [B] [C] [D]  **31.** [A] [B] [C] [D]  **32.** [A] [B] [C] [D]

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa



CamScanner

**Swali la 1 hadi la 5.**

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.**

**Amani** : Hujambo Juma! Habari ya leo?

**Juma** : Sijambo Amani. Asante kuuliza. Na wewe je?

**Amani** : Mimi niko vizuri. Juma, nataka kukuuliza jambo. Kwa nini ni muhimu kusema *tafadhali* na *asante*?

**Juma** : Hii ni rahisi. Tunaposema *tafadhali* tunamuonyesha mtu kwamba tunamheshimu, na *asante* tunaonyesha ishara ya shukrani.

**Amani** : Ndiyo, hiyo ni kweli. Na pia, tunapaswa kumheshimu mtu yeyote aliyetuzidi kiumri kama wazazi au walimu.

**Juma** : Sahihi kabisa. Kwa mfano, kumwambia mwalimu *samahani, naomba nifanye* badala ya kusema kwa ghafla bila heshima.

**Amani** : Kumsikiliza mtu anapozungumza pia ni adabu. Hii inaonyesha tunamheshimu.

**Juma** : Kweli kabisa! Hivyo basi, adabu si maneno tu, bali na pia ni tabia inayokubalika nzuri.

**Amani** : Ndio, Juma. Tukiendelea hivyo, tutakuwa na marafiki wengi na watu watatuheshimu.

**Juma** : Ni kweli , Amani. Hebu tukumbushane kila siku kuhusu heshima na adabu!

**1.** Juma na Amani walizungumza kuhusu nini?

A. Michezo B. Lugha ya heshima na adabu
C. Chakula cha shule D. Mavazi shuleni

**2.** Ni neno lipi linaloonyesha unyenyekevu unapomuuliza mtu jambo?

A. Samahani B. Haraka
C. Tafadhali D. Sema

**3.** Kwa nini Amani anasema ni muhimu kuheshimu mtu mkubwa kuliko wao?

A. Ili awe rafiki kwao B. Ili apate zawadi
C. Ili kumchekesha D. Ili kuonyesha heshima

**4.** Juma anasema kuwa ; adabu ni________________

A. tabia nzuri na maneno ya heshima B. maneno tu
C. kucheka mara kwa mara D. kuongea kwa sauti kubwa



CamScanner

5. Juma na Amani walipendekeza kufanya nini kila siku?

A. Kusoma vitabu vya hadithi

B. Kukumbushana kuhusu heshima na adabu

C. Kucheza mpira wa kandanda

D. Kufanya kazi za shule bila kusikiliza

**Swali la 6 hadi la 9**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Katika msitu wenye miti mirefu na majani mapana, Nyani alikuwa akiruka kutoka tawi moja hadi jingine akitafuta matunda. Akielekea kwenye mti wa matunda alioupenda, aliona Kijito kidogo mbele yake kimetawanyika na mawe madogo.

Nyani aliona Kuku Mdogo akiwa kando ya kijito hicho, akihangaika kutafuta njia ya kuvuka bila kulowesha manyoya yake. Kijito kilikuwa na mtiririko wa kasi ambao ungeweza kumvuta kirahisi kama angejaribu kuvuka peke yake.

Nyani alisimama kwa muda mfupi akafikiria. Kisha akakusanya matawi makavu na kuyaweka juu ya mawe makubwa, akatengeneza daraja dogo la kuvukia. Kuku akavuka taratibu hadi upande wa pili bila hatari yoyote.

Kuku alipofika salama upande mwingine, Nyani aliendelea na safari yake kuelekea mti wa matunda. Alipofika, aligundua kuwa mti huo ulikuwa na matunda machache kuliko siku zilizopita, lakini hakujuta kamwe kucheleweshwa. Alijisikia vizuri kwa sababu alisaidia kiumbe mwingine.

6. Nyani alikuwa akitafuta nini wakati alikutana na Kuku Mdogo?

A. Chakula cha majira ya joto

B. Matunda

C. Maji ya kunywa

D. Kijito kipya

7. Tatizo la Kuku Mdogo lilikuwa nini?

A. Kijito kilikuwa kimemnyima usalama na alikuwa hatarini kuanguka

B. Kuku Mdogo alikuwa amepotea kwenye msitu

C. Kuku Mdogo alikuwa hajui kuvuka

D. Kijito kilikuwa kimejaa matunda



CamScanner

**8.** Nyani alitengeneza njia ya jinsi gani kumsaidia Kuku Mdogo?

A. Akamwongoza kwenye njia mrefu

B. Alikusanya matawi na kuyaweka juu ya mawe ili kuunda daraja dogo

C. Akampeleka akimkimbiza

D. Akampaka maji ili atembee taratibu

**9.** Mafunzo makuu ya kisa hiki ni:

A. Hatua ndogo za wema zina thamani

B. Kusaidia wengine huwezi kufanikisha chochote

C. Wema huja tu kwa maneno

D. Kila mmoja lazima akusanye matunda

**Swali la 10 hadi la 12**

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.</u>**

Katika pori la mwangaza, Wanyama waliishi kama familia moja kwa ushirikiano na upendo. Kati yao alikuwepo fisi korongo, kiumbe mwenye kicheko cha ajabu kilichotangulia hata kama hajaonekana. Ingawa alionekana mcheshi kupita kiasi, alikuwa mlinzi shupavu wa pori, alihakikisha hakuna hatari iliyokaribia bila kugunduliwa.

Siku moja, ngiri mmoja mwenye roho safi alipotea kwenye vichaka. Wanyama walihangaika, kila mmoja akichangia kwa njia yake kumtafuta. Swara alitumia wepesi wake kumtafuta kwa kasi, huku Tai akipaa juu akichunguza dunia kama amani iliyotandazwa. Hatimaye, walimkuta ngiri amelala usingizi mzito chini ya mti wa mkuyu baada ya kuchoka. Walicheka kwa Pamoja, wakitambua kuwa kila mmoja alikuwa muhimu katika kuleta amani na umoja wa pori.

**10.** Fisi korongo alikuwa na tabia gani ya pekee?

A. Alikuwa mwenye sauti ya kutisha

B. Alikuwa na kicheko cha ajabu

C. Alikuwa mkimya sana

D. Alipenda kulala sana

**11.** Wanyama katika pori ya mwangaza walihangaika kumtafuta nani?

A. Tai

B. Swara

C. Kobe

D. Ngiri



CamScanner

12. Tai alitoa mchango gani katika utafutaji?

A. Alipiga kelele

B. Alitembea polepole ardhini

C. Alipaa juu hewani kuangalia eneo

D. Alimwita Ngiri kwa sauti kubwa

**Swali la 13 hadi la 15**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Uandishi wa insha ni njia ya kueleza mawazo na hisia zako kwa maneno. Kila mwanafunzi anapopata karatasi na kalamu, ana nafasi ya kuandika kile alichojifunza, kile anachokiona, na kile anachokihisi. Kuandika insha kunasaidia pia kukuza akili na kuongeza ujuzi wa lugha.

Ili kuandika insha nzuri, mwanafunzi anapaswa kuwa na mpangilio mzuri. Anaweza kuanza kwa utangulizi unaoeleza mada, kisha kuandika aya za katikati zinazotoa maelezo au mifano, na kumalizia na hitimisho linalofupisha mawazo yake. Kwa kufanya hivi, insha yake itakuwa rahisi kueleweka na kuvutia wasomaji.

13. Uandishi wa insha husaidia mwanafunzi kuonyesha nini?

A. Uchovu wa mwili

B. Mawazo na hisia zake

C. Rangi ya penseli

D. Mwendo wa kuandika na kusoma

14. Ni jambo gani linapaswa kufanywa kwanza wakati wa kuandika insha?

A. Kuandika hitimisho

B. Kueleza mada kwa utangulizi

C. Kuandika aya za katikati

D. Kusoma gazeti

15. Hitimisho la insha linapaswa kufanya nini?

A. Kutoa muhtasari wa mawazo yote ya mwandishi

B. Kuongeza vitabu kwenye maktaba

C. Kufundisha wengine kucheza soka

D. Kuandika yatakayojiri



CamScanner

**Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo kati ya yale uliyopewa.**

Kila siku, ndugu wawili huenda shambani ili____16____mimea na matunda. Shambani, kuna aina nyingi ____17____ mimea kama vile mikunde, maboga na nyanya. Wanaweza pia kuwaona ____18____ wanaokula majani ya mimea hiyo. Baada ya kazi shambani, mimi huenda nyumbani ____19____ maji na kula chakula cha mchana. Ni muhimu pia kupumzika kwa muda____20____ kupata nguvu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | **A.** kukata | **B.** kuvuna | **C.** kupanda | **D.** kuchafua |
| **17.** | **A.** ya | **B.** za | **C.** kwa | **D.** la |
| **18.** | **A.** wadudu | **B.** wanyama | **C.** ndege | **D.** pori |
| **19.** | **A.** kula | **B.** kunywa | **C.** kumwaga | **D.** kuteka |
| **20.** | **A.** ili | **B.** sababu | **C.** sembuse | **D.** pia |

**Kutoka swali la 21 hadi 30, chagua jibu sahihi.**


**21.** Wingi wa nomino ubao ni ______________.

A. mabao
B. bao
C. vibao
D. mibao

**22.** Akisami $\frac{1}{3}$ huitwa?

A. Theluthi
B. Robo
C. Nusu
D. Humusu

**23.** Umbo hili huitwa ______________________.



A. Pia
B. Tao
C. Duara
D. Mcheduara

**24.** Sehemu katikati ya jicho huitwa _______________

A. pua
B. mboni
C. kisogo
D. kisugudi



CamScanner

25. Pambo linalovaliwa hasa na wanawake shingoni huitwa ________________

A. pete
B. mkufu
C. bangili
D. kipuli

26. Iwapo leo ni Jumatatu , je, mtondo itakuwa siku gani?

A. Jumanne
B. Jumatatu
C. Ijumaa
D. Alhamisi

27. Jibu sahihi la maamkuzi chewa ni?

A. Binuru
B. Aheri
C. Chewa
D. Salama

28. **Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kiambishi kifaacho**

Alisafiri__________ gari la moshi hadi Kisumu.

A. na
B. kwa
C. la
D. cha

29. Tarakimu " **elfu mia tano sitini na saba, mia saba tisini na moja"** kwa nambari ni______________.

A. 567,791
B. 597,761
C. 567,667
D. 597,767

30. Ni sentensi ipi iliyo katika wakati uliopita?

A. Baba atasoma gazeti hiyo
B. Mama alipika wali
C. Yona anaimba vizuri
D. Farida atatuzwa kesho.



CamScanner

# TARGETER WINGS
# KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
# GREDI YA 6 - MWAKA WA 2026
## SEHEMU B:
## KISWAHILI INSHA

Wings 001

***MUDA:* *Dakika 40***

| | |
|---|---|
| **JINA LAKO** | |
| **JINA LA SHULE YAKO** | |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd. Email:info@targeterpublishers.co.ke*



CamScanner

*Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.*

**Andika kisa cha kusisimua kuhusu:**

## HARUSI NILIYOHUDHURIA